/ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 50*** ***20th December, 2024***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No.47 Vol. 105 Dated 20th December, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI Na. 1080 la tarehe 20/12/2024

SHERIA YA BENKI KUU YA TANZANIA
(SURA YA 197)

# NOTISI

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 26 na 27(2))*

NOTISI YA BENKI KUU YA TANZANIA (INGIZO LA CHAPISHO LA NOTI KWENYE MZUNGUKO LENYE MAREJEO YA TOLEO LA MWAKA 2010) YA MWAKA 2024

Jina

**1**. Notisi hii itajulikana kama Notisi ya Benki Kuu ya Tanzania (Ingizo la Chapisho la Noti kwenye Mzunguko lenye Marejeo ya Toleo la Mwaka 2010) ya mwaka 2024.

Ingizo kwenye mzunguko Chapisho la Noti
Sura ya 197

**2**.-(1) Katika kutekeleza mamlaka iliyopewa Benki Kuu ya Tanzania na vifungu vya 26 na 27(2) vya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Benki inautaarifu umma kuwa kuanzia tarehe ya kuchapishwa kwa Notisi hii, imeingiza kwenye mzunguko Chapisho la Noti za Shilingi Elfu Moja, Elfu Mbili, Elfu Tano na Elfu Kumi lenye Marejeo ya Toleo la Mwaka 2010.

(2) Noti za Shilingi Elfu Moja, Elfu Mbili, Elfu Tano na Elfu Kumi za toleo la mwaka 2010 zilizopo kwenye mzunguko zitaendelea kutumika kama noti halali kwa malipo sambamba na chapisho linaloingizwa kwenye mzunguko likirejea toleo la Mwaka 2010.

Sifa za Chapisho linaloingizwa kwenye mzunguko

**3**. Chapisho la Noti za Shilingi Elfu Moja, Elfu Mbili, Elfu Tano na Elfu Kumi zina sifa sawa na Toleo la Mwaka 2010 na sahihi ya Waziri wa Fedha na Gavana wa

Benki Kuu ya Tanzania kama ilivyoainishwa katika Jedwali.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)*

SIFA ZA CHAPISHO LENYE MAREJEO YA TOLEO LA MWAKA 2010

| UPANDE WA NOTI | A: SIFA ZA UJUMLA ZILIZOPO KWENYE NOTI ZOTE |
|---|---|
| UPANDE WA MBELE | 1. Upande wa pembeni-katikati unaoonyesha Nembo ya Taifa. |
| | 2. Juu ya katikati ya noti na juu ya motifu kuu kuna maneno yanayosomeka "BENKI KUU YA TANZANIA" na kifungu cha ahadi ya malipo kwa noti husika. |
| | 3. Chini ya motifu kuu ni sahihi ya Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Waziri wa Fedha na Emmanuel Mpawe Tutuba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania. |
| | 4. Eneo ambalo halijachapishwa upande wa kushoto wa noti lina alama ya kivuli kilichojificha cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na thamani ya noti husika, ikielekezwa kwenye mwanga. |
| | 5. Noti ina namba mbili zinazofanana zenye muundo wa herufi mbili na tarakimu saba; moja kwa mlalo upande wa chini kushoto na nyingine wima kwenye ukingo wa kulia wa noti. |
| | 6. Alama za vipande vipande zenye kuonesha thamani ya noti husika inapomulikwa kwenye mwanga ambapo tarakimu za thamani ya noti husika hutokea. |
| | 7. Alama ya wino maalum uliofichika upande wa kushoto wa noti ambayo huonesha thamani ya noti husika na kifupisho cha Shillingi ya Tanzania "TZS" noti ikimulikwa kwa mwanga maalum wa rangi ya zambarau kwa noti za 2000, 5000 na 10000. Vile vile, kwa noti ya 1000 alama ya wino maalum uliofichika huonekana upande wa kushoto wa motifu kuu ikionesha thamani ya noti husika pindi noti ikimulikwa kwa mwanga maalum wa zambarau. |
| | 8. Maandishi madogo sana yaliyolala na kutuna yanayoonekana kwa kutumia vifaa maalum vya kukuzia maandishi. |
| | 9. Kivuli kilichofichika upande wa kushoto wa motifu kuu chenye kuonesha thamani ya noti husika ambayo huonekana kuwa angavu noti inapogeuzwageuzwa. |

| | |
|---|---|
| | 10. Utepe mwembamba wa kiusalama upande wa kulia wa noti unaonesha kutembea na kubadilika kwa rangi. Rangi za utepe zinaonesha upinde wa mistari mithili ya mawimbi yanayotembea kutoka kushoto kwenda kulia na kinyume chake pale noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini. Pia, inapoelekezwa kwenye mwanga maneno "BOT 2000", "BOT 5000" na "BOT 10000" yanasomeka kwa noti za 2000, 5000 na 10000. |
| | 11. Chapisho la motifu Kuu, Nembo ya Taifa, Thamani ya noti, maneno "BENKI KUU YA TANZANIA", Maandishi madogo sana, Alama za Utambuzi wa noti kwa wenye uoni hafifu zimechapishwa kwa kutuna na kuparuza. |
| | 12. Nyuzi nyembamba zenye rangi nyekundu na bluu kwenye noti ambazo huonekana kwenye mwanga wa kawaida na Nyuzi nyembamba zenye rangi nyekundu, bluu na kijani zilizofichika ambazo huonekana kwa kutumia mwanga maalum wa rangi ya zambarau. |
| | |
| UPANDE WA NYUMA | 1. Kila noti ina picha yake mahsusi. |
| | 2. Maneno yanayosomeka "BANK OF TANZANIA" yamechapishwa kwenye upande wa kushoto, juu ya noti. |
| | 3. Alama ya wino maalum uliofichika iliyopo katikati ya noti ambayo huonesha rangi mbili pindi noti ikimulikwa kwa mwanga wa rangi ya zambarau kwenye noti ya 2000, 5000 na 10000. |
| | 4. Namba ya thamani ya noti husika imechapishwa kwenye upande wa juu kulia na pembe ya chini kushoto. |
| | 5. Maandishi ya thamani ya noti husika yameandikwa kwa Kiingereza na yamechapishwa kwa herufi kubwa kwenye pembe ya chini upande wa kulia. |
| | 6. Alama maalum ya Twiga inaonekana ndani yenye rangi ya dhahabu juu kidogo katikati ya noti upande wa kulia ambayo hubadilika kuwa rangi ya kijani na kurudia tena kuwa ya dhahabu noti inapogeuzwa kwa noti ya 2000, 5000 na 10000. |
| | 7. Nyuzi nyembamba zenye rangi nyekundu na bluu kwenye noti ambazo huonekana kwenye mwanga wa kawaida na Nyuzi nyembamba zenye rangi nyekundu, bluu na kijani zilizofichika ambazo huonekana kwa kutumia mwanga maalum wa rangi ya zambarau. |
| | |
| B: SIFA MAHSUSI | |
| TZS 1000<br>Ukubwa: 125 x 65mm Rangi: Bluu Dhima: Rasilimali Asili na Kilimo | |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL

| | |
|---|---|
| UPANDE WA MBELE | 1. Alama ya mguso inayoparuza ya picha rasmi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katikati ya nusu ya kulia ya noti. |
| | 2. Alama ya mguso inayoparuza inayotambulisha thamani ya noti kwa kuipapasa kwa watu wenye uoni hafifu iliyowasilishwa kama mistari miwili mikubwa iliyo sambamba iliyowekwa kwenye kona ya chini kushoto. |
| | 3. Alama maalum upande wa kulia wa noti inayoonesha tarakimu 1000 na kichwa cha twiga, noti ikiangaliwa sambamba usawa wa macho. |
| | |
| UPANDE WA NYUMA | 1. Alama ya mguso inayoparuza ya picha ya Ikulu ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, mimea ya kahawa na karafuu inayoonekana upande wa katikati-kushoto wa noti. |
| | 2. Uzi mwembamba upande wa kulia wa noti wenye ukubwa wa 2mm na maandishi “BOT 2023” yanayojirudia na kuonekana noti ikiwa imekingwa kwenye mwanga. |
| | 3. Alama maalum yenye kichwa cha Twiga ndani yake upande wa kulia wa noti. |
| | 4. Mkanda unaong’aa ulio katikati ya noti ukionesha tarakimu ya thamani ya noti 1000 inayojirudia. |
| | |
| TZS 2000<br>Ukubwa: 130 x 66mm Rangi: Hudhurungi Dhima: Utalii na Utamaduni | |
| UPANDE WA MBELE | 1. Alama ya mguso inayoparuza yenye picha inayoonesha kichwa cha simba iliyo upande wa katikati-kulia kwa noti. |
| | 2. Alama ya mguso inayotambulisha thamani ya noti kwa kuipapasa kwa watu wenye uoni hafifu iliyo upande wa chini kushoto kama mistari miwili inayounda umbo linalofanana na ‘V’ iliyo kinyume (iliyogeukia chini). |
| | 3. Utepe wa usalama wenye ukubwa wa 4.0mm unaoonesha kutembea na kubadilika kwa rangi. Rangi za utepe huo zinaonesha upinde wa mistari mithili ya mawimbi yanayotembea kutoka kushoto kwenda kulia na kinyume chake, pale noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini. Rangi za utepe huo zinabadilika toka rangi ya dhahabu kuwa kijani. Noti unapoielekeza kwenye mwanga kuna maneno yanayosomeka: “BOT 2000”. |
| | |
| UPANDE WA NYUMA | 1. Alama ya mguso inayoparuza iliyo katikati-kushoto kwa noti inayoonesha picha ya Ngome Kongwe ya Zanzibar. |
| | 2. Alama ya mguso inayoparuza iliyo katikati ya noti na pembeni ya Ngome Kongwe ya Zanzibar inayoonesha sanduku lenye asili ya Zanzibar. |
| | 3. Alama ya mng’ao ya rangi ya dhahabu ambayo inabadilika kuwa kijani na kurudia kuwa rangi ya dhahabu. |
| | |

*Tangazo la Serikali Na.1080 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| TZS 5000<br>Ukubwa: 135 x 67mm Rangi: Zambarau Dhima: Madini na Viwanda | |
| UPANDE WA MBELE | 1. Alama ya mguso inayoparuza katikati upande wa kulia wa noti inayoonesha picha ya kichwa cha Kifaru. |
| | 2. Alama ya mguso inayotambulisha thamani ya noti kwa kuipapasa kwa watu wenye uoni hafifu iliyo upande wa chini kushoto iliyowasilishwa kama mistari miwili inayounda maumbo mawili yanayofanana na 'V' iliyo kinyume (iliyogeukia chini). |
| | 3. Utepe wa usalama wenye ukubwa wa 4.5mm unaoonesha kutembea na kubadilika kwa rangi. Rangi za utepe huo zinaonesha upinde wa mistari mithili ya mawimbi yanayotembea kutoka kushoto kwenda kulia na kinyume chake noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini. Rangi za utepe huo zinabadilika toka rangi ya bluu kwenda zambarau. Noti unapoielekeza kwenye mwanga, kuna maneno yanayosomeka: "BOT 5000". |
| | |
| UPANDE WA NYUMA | 1. Alama ya mguso inayoparuza iliyo katikati ya noti inayoonesha kiwanda cha Ashanti Goldmine. |
| | 2. Alama ya mng'ao ya rangi ya dhahabu ambayo inabadilika kuwa kijani na kurudia kuwa rangi ya dhahabu. |
| | |
| TZS 10000<br>Ukubwa: 140 x 68mm Rangi: Nyekundu Dhima: Huduma za Fedha | |
| UPANDE WA MBELE | 1. Alama ya mguso inayoparuza iliyopo katikati upande wa kulia wa noti inayoonesha kichwa cha Tembo. |
| | 2. Alama ya mguso inayotambulisha thamani ya noti kwa kuipapasa kwa watu wenye uoni hafifu iliyo upande wa chini kushoto iliyowasilishwa kama mistari miwili inayounda maumbo matatu yanayofanana na 'V' iliyo kinyume (iliyogeukia chini). |
| | 3. Utepe wa usalama wenye ukubwa wa 4.5mm unaoonesha kutembea na kubadilika kwa rangi. Rangi za utepe huo zinaonesha upinde wa mistari mithili ya mawimbi yanayotembea kutoka kushoto kwenda kulia na kinyume chake, pale noti hiyo inapogeuzwageuzwa upande au juu na chini. Rangi za utepe huo zinabadilika toka rangi ya pinki kwenda kijani. Noti unapoielekeza kwenye mwanga, yanaonekana maneno yanayosomeka: "BOT 10000". |
| | |

*Tangazo la Serikali Na.1080 (Linaendelea.)*

| | |
|---|---|
| UPANDE WA NYUMA | 1. Alama ya mguso inayoparuza iliyopo upande wa kushoto wa noti, inayoonesha majengo ya Benki Kuu Makao Makuu ndogo ya Dar es Salaam. |
| | 2. Alama ya mng'ao ya rangi ya dhahabu ambayo inabadilika kuwa kijani na kurudia kuwa rangi ya dhahabu. |

Dodoma,
17 Desemba, 2024

EMMANUEL M. TUTUBA,
*Gavana*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA